



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO**

**MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU YA
MBOLEA KWA MSIMU WA 2026/2027**

JUNI, 2026

YALIYOMO

YALIYOMO	2
DIBAJI	Kosa! Kiashiri mada hakikufasiliwa.
1.0 UTANGULIZI.....	4
1.1.Chimbuko na msingi wa Kisheria wa Mwongozo	4
1.2.Lengo Kuu la Mwongozo.....	5
1.3.Malengo Mahsusi	5
2.0 UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU.....	5
2.1 Usajili/Uhuishaji wa Taarifa za Wakulima	5
2.2 Usajili na Uhuishaji wa Taarifa za Waingizaji/ Wazalishaji wa Mbolea	6
2.3 Usajili na Uhuishaji wa Taarifa za Mawakala wa Mbolea	7
2.4 Vigezo vya kunufaika na Ruzuku (Eligibility Criteria).....	7
2.5 Bei elekezi za mbolea katika Mpango wa Ruzuku.....	8
2.6 Usambazaji na Uuzaji wa Mbolea kwa Wakulima	8
2.7 Utoaji wa Elimu na Mafunzo kwa Wadau.....	8
2.8 Usimamizi wa Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea	8
2.9 Mawanda ya Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kwa Wakulima.....	9
2.10 Utoaji wa Adhabu.....	9
2.11 Utaratibu wa malipo ya ruzuku ya mbolea iliyosambazwa kwa wakulima	10
3.0 MUUNDO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU.....	10
3.1 Utaratibu wa utoaji wa Ruzuku kupitia mfumo wa Kidijitali (<i>Agricultural Inputs Subsidy System</i>)	11
3.2 Muundo wa Usimamizi na Uendeshaji.....	13
3.2.1.Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea	13
3.2.2.Kamati ya Taifa ya Ufuatiliaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea	14
3.2.3.Kamati Tendaji (Technical Committee)	14
4.0 NGAZI ZA UTEKELEZAJI NA WAJIBU WA WADAU	15
4.1 Wizara ya Kilimo	15
4.2 Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)	15
4.3 Bodi za Mazao na Wakala ya Taifa ya Huduma za Ugani (NAESA).....	16
4.4 Sekretarieti za Mikoa	17
4.5 Mamlaka za Serikali za Mitaa	17
4.6 Waingizaji/ Wazalishaji wa Mbolea	18
4.7 Mawakala (Agrodealers) wa Mbolea.....	18
4.8 Taasisi za Fedha	19
4.9 Wakulima.....	19
5.0 MAMBO YA KUZINGATIA	20
6.0 MAREKEBISHO.....	20
7.0 HITIMISHO	21

DIBAJI

Katika msimu wa 2026/2027, Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kwa lengo la kupunguza gharama ya mbolea kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda. Utoaji wa ruzuku unazingatia mahitaji ya mkulima kulingana na taarifa za usajili na bajeti ya Serikali iliyotengwa.


Mpango huu unahusisha mbolea za kupandia na kukuzia. Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (Tanzania Fertilizer Regulatory Authority- TFRA) itatoa orodha ya mbolea zinazohusika kwenye mpango wa ruzuku. Katika mpango wa ruzuku, mkulima ananunua mbolea kwa bei ya ruzuku kulingana na ukubwa wa shamba na aina ya zao. Aidha, Wazalishaji wa Mbolea wa ndani pamoja na kushiriki katika mpango huu wa ruzuku, wanashiriki pia katika Mpango Maalumu wa Ruzuku kwa Wazalishaji wa Mbolea nchini.

Wizara ya Kilimo kupitia TFRA inaendelea kutumia mfumo wa kidijitali katika kutoa ruzuku ya mbolea ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa ruzuku; kupunguza mianya ya udanganyifu na gharama za usimamizi. Mfumo huo unatumia programu maalum ya kidijitali kusajili wakulima, waingizaji/wazalishaji wa mbolea, mawakala pamoja na kuratibu usambazaji wa mbolea kwa wakulima na malipo ya ruzuku ya mbolea.

Utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea unasimamiwa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo, Wizara ya Fedha, TFRA, Bodi za Mazao, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Waingizaji/Wazalishaji wa Mbolea, Mawakala (Agrodealers) wa Mbolea, Taasisi za Fedha, Wakulima na wadau wengine. Kutokana na kuwepo kwa wadau mbalimbali, Wizara huandaa mwongozo maalum kwa ajili ya kurahisisha uratibu wa mpango huo.

Mwongozo huu unaainisha utaratibu wa utoaji na usimamizi wa ruzuku ya mbolea ikiwa ni pamoja na usajili wa wakulima, waingizaji/wazalishaji, wasambazaji wa mbolea, ngazi za utekelezaji, mawanda ya ruzuku na wajibu wa wadau katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kwa msimu wa 2026/2027.

Ninatoa wito kwa wadau wa Sekta ya Kilimo nchini kutumia Mwongozo huu ili kurahisisha uratibu na kutambua wajibu wa kila mdau katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.



Gerald G. Mwel, *ndc*

KATIBU MKUU

1.0 UTANGULIZI

Serikali inatekeleza Mpango wa Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea kwa wakulima kwa lengo la kupunguza gharama ya mbolea ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda.

Katika msimu wa 2021/2022, Sekta ya Kilimo ilikabiliwa na changamoto ya kupanda kwa bei ya mbolea katika soko la ndani kutokana na kupanda kwa bei ya mbolea katika soko la dunia. Kupanda kwa bei kulisababishwa na athari ya UVIK0-19 pamoja na vita ya Ukraine na Urusi. Hali hiyo ilichangia kushuka kwa matumizi ya mbolea, tija na uzalishaji. Kuanzia msimu wa 2022/2023, v Serikali ilianza kutekeleza mpango wa ruzuku ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa wakati. Utekelezaji wa mpango huo umechangia kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kwa wakulima kutoka tani 363,599 (2021/2022) hadi tani 972,074 (2024/2025).

Aidha, katika msimu wa 2025/2026 kumetokea changamoto ya mgogoro katika eneo la Mashariki ya Kati ambao umeathiri uzalishaji na usafirishaji wa mbolea hasa za nitrojeni katika soko la Dunia. Hali hiyo imesababisha kupanda kwa bei za mbolea na nishati ya mafuta katika soko la Dunia na hivyo kuathiri bei katika soko la ndani. Changamoto hiyo, imeongeza hitaji la Serikali kutoa ruzuku ili kuwawezesha wakulima kupata mbolea kwa bei himilivu.

Serikali imepanga kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea kwa mwaka 2026/2027 ili kuongeza tija katika kilimo, kuongeza uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula nchini na kukidhi mahitaji ya masoko ya ndani na kimataifa. Aidha, utoaji wa ruzuku unazingatia mahitaji halisi ya mkulima kulingana na taarifa za usajili na bajeti ya Serikali iliyotengwa.

1.1. Chimbuko na msingi wa Kisheria wa Mwongozo

Serikali imeandaa Mwongozo huu ili kuhakikisha usimamizi bora, uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea. Lengo ni kulinda wakulima na kuimarisha sekta ya kilimo kwa kuhakikisha ruzuku ya mbolea inawafikia walengwa sahihi na kupunguza mianya ya udanganyifu.

Aidha, Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia Kifungu cha 4(1)(o) cha Sheria ya Mbolea, Sura ya 378, kinachotoa mamlaka kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuweka utaratibu wa kusimamia mpango wa ruzuku. Hivyo, mwongozo huu ni nyenzo inayoweza uratibu wa utekelezaji wa mpango huo kwa manufaa ya wakulima na maendeleo endelevu ya kilimo nchini.

1.2. Lengo Kuu la Mwongozo

Mwongozo wa Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kwa msimu wa kilimo 2026/2027 umelenga kutoa utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima na wadau wa kilimo.

1.3. Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya Mwongozo ni:-

- i. Kuimarisha udhibiti na ufuatiliaji wa usambazaji wa mbolea kwa wakati katika maeneo ya uzalishaji ili kuleta ufanisi na uwajibikaji;
- ii. Kuainisha Mawanda ya Ruzuku ya mbolea itakayotolewa kwa wakulima; na
- iii. Kuainisha ngazi za utekelezaji na wajibu wa wadau katika usimamizi wa utoaji wa ruzuku ya mbolea.

2.0 UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU

Utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea unahusisha taratibu zifuatazo:-

2.1 Usajili/Uhuishaji wa Taarifa za Wakulima

Wakulima, Vikundi vya Wakulima, Vyama vya Ushirika, Taasisi na Kampuni zinazojishughulisha na kilimo lazima wajasajili ili kuweza kununua mbolea. Kila aliyesajiliwa atapewa namba maalumu ya utambulisho. Aidha, taarifa za usajili wa wakulima zinaweza kuhuishwa wakati wowote endapo mkulima atahitaji kubadili ukubwa shamba, nambari ya simu na aina ya zao.

Usajili na uhuishaji wa taarifa za wakulima ambao walisajiliwa katika misimu iliyopita unafanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ngazi ya vijiji/mitaa kwa kuingiza taarifa za

wakulima kama ifuatavyo:-

A. Wakulima Binafsi

- (i) Jina kamili la mkulima;
- (ii) Mahali anapoishi (Kijiji/Mtaa);
- (iii) Jinsi (Me/Ke);
- (iv) Namba ya simu;
- (v) Kitambulisho cha Taifa au Mpiga Kura ;
- (vi) Nambari ya kitambulisho;
- (vii) Tarehe ya kuzaliwa;
- (viii) Ukubwa wa shamba (ekari/GPS);
- (ix) Aina ya mazao;
- (x) Kikundi cha mkulima (AMCOS au Kikundi cha kijiji); na
- (xi) Picha ya Pasipoti/Alama ya kidole.

B. Taasisi, Kampuni na Vikundi vya wakulima vilivyosajiliwa

- (i) Jina la Taasisi/Kampuni/Kikundi/Chama;
- (ii) Mahali Taasisi/Kampuni/Kikundi/Chama kilipo (Mkoa, Wilaya Kata na Kijiji);
- (iii) Namba ya Simu ya Taasisi/Kampuni/Kikundi/Chama;
- (iv) Anuani ya baruapepe ya Taasisi/Kampuni/Kikundi/Chama (kama ipo); na
- (v) Namba ya usajili kutoka Mamlaka inayohusika.

Mkulima aliyesajiliwa/kuhuisha taarifa zake atapokea ujumbe mfupi kwenye simu yake kumtaarifu kukamilika kwa zoezi hilo na atapewa namba ya utambulisho ambayo ataitumia kununua mbolea kwa wakala.

ANGALIZO: Kila mkulima atakayesajiliwa anapaswa kuwa na namba yake ya simu wakati wa usajili na ndiyo itapokea namba ya utambulisho wa mkulima atakayotumia kununua mbolea. Mkulima hataruhusiwa kutumia namba ya simu ya mtu mwingine wakati wa usajili/kununua mbolea.

2.2 Usajili na Uhuishaji wa Taarifa za Waingizaji/ Wazalishaji wa Mbolea

Muingizaji/Mzalishaji wa Mbolea atakayeshiriki katika usambazaji wa mbolea katika mpango wa ruzuku atapaswa kufuata hatua zifuatazo:-

- (i) Kujisajili kushiriki mpango wa ruzuku kwa kuwasilisha taarifa zifuatazo:-
 - a) Namba ya leseni ya kufanya biashara ya mbolea; na
 - b) Taarifa za akaunti ya Benki itakayotumika.
- (ii) Kuhuisha taarifa zake zilizosajiliwa kwenye mfumo misimu iliyopita; na
- (iii) Kuwasilisha kwa TFRA taarifa za mawakala wake na vituo vya usambazaji wa mbolea katika kila Mkoa au Wilaya anakotoa huduma.

Aidha, TFRA itachambua maombi na kutoa mrejesho kwa muombaji. Iwapo muombaji atakuwa amekidhi vigezo atasajiliwa na kupewa namba maalum ya utambulisho na kusaini mkataba.

2.3 Usajili na Uhuishaji wa Taarifa za Mawakala wa Mbolea

Usajili wa mawakala utafanywa na TFRA kwa kuzingatia orodha iliyowasilishwa na waagizaji/wazalishaji wa mbolea. Mawakala wa mbolea watakaoshiriki kusambaza mbolea katika mpango wa ruzuku watapaswa kufuata hatua zifuatazo:-

- (i) Kujisajili kushiriki mpango wa ruzuku kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-
 - (a) kuwa na namba ya leseni ya kufanya biashara ya mbolea; na
 - (b) kuwa na uthibitisho wa kuteuliwa na kampuni (waingizaji/wazalishaji) kwa ajili ya kusambaza na kuuza mbolea katika mpango wa ruzuku;
- (ii) Kuhuisha taarifa zake zilizosajiliwa kwenye mfumo katika misimu iliyopita; na
- (iii) Kuainisha vituo vya mauzo ya mbolea katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Kijiji.

2.4 Vigezo vya kunufaika na Ruzuku ya mbolea

Mwongozo huu unaainisha vigezo vitakavyozingatiwa ili mkulima aweze kunufaika na ruzuku ya mbolea. Ili kuhakikisha uwazi na uendelevu wa zoezi hili, kila mnufaika anatakiwa kutimiza masharti yanayobainisha sifa za msingi za kustahiki. Vigezo hivyo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Awe amesajiliwa katika Mfumo wa Usajili wa Wakulima na kupata namba ya Mkulima.

- (ii) Awe na ukubwa wa shamba ulioainishwa kwenye mawanda ya ruzuku katika mwongozo huu; na
- (iii) Awe analima mazao ya kilimo kama ilivyoainishwa kwenye mawanda ya ruzuku katika mwongozo huu.

2.5 Bei elekezi za mbolea katika Mpango wa Ruzuku ya Mbolea

Bei elekezi ya mbolea ya ruzuku itapangwa na TFRA kwa kuzingatia mwenendo wa bei ya mbolea katika soko la Dunia, gharama za uzalishaji na utaratibu ulioainishwa katika kanuni ya 42 ya Kanuni za Mbolea za mwaka 2026 kulingana na mahitaji ya wakati huo. Mbolea zitauzwa kwa wakulima katika mpango wa ruzuku kwa bei itakayotangazwa na TFRA kulingana na aina ya mbolea na kwa kuzingatia umbali kutoka kwenye ghala la muingizaji au mzalishaji.

2.6 Usambazaji na uuzaji wa mbolea kwa wakulima

Usambazaji na uuzaji wa mbolea utafanywa na Kampuni za Mbolea kupitia vituo vya mauzo, Vyama vya Ushirika na mawakala walioteuliwa na Kampuni husika. Kampuni zinapaswa kuhakikisha mawakala walioteuliwa wana mbolea za kutosha wakati wote wa msimu kulingana na mahitaji. Aidha, usambazaji, uhifadhi na uuzaji wa mbolea unapaswa kuzingatia utaratibu ulioainishwa katika kanuni ya 32 (2) ya Kanuni za Mbolea za mwaka 2026.

2.7 Utoaji wa Elimu na Mafunzo kwa Wadau

Utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima utahusisha utoaji wa elimu na mafunzo kwa wadau mbalimbali watakaoshiriki katika mpango wa ruzuku. Kila ngazi ya utekelezaji ina jukumu la kutoa elimu kwa wadau kuhusu mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima.

2.8 Usimamizi wa Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea

Mpango wa ruzuku ya mbolea utasimamiwa na Wizara ya Kilimo kupitia TFRA kwa kushirikiana na Sekritarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kamati ya Taifa ya Ufuatiliaji wa Ruzuku ya Mbolea.

2.9 Mawanda ya Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kwa Wakulima

Mawanda ya ruzuku kwa wakulima katika msimu wa 2026/2027 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Ruzuku itatolewa kwa wakulima wanaomiliki shamba au mashamba yenye jumla ya ekari zisizozidi 50 nchini;
- (ii) Wakulima wanaomiliki zaidi ya ekari 50 watanunua mbolea hizo kwenye mfumo na kwa bei ya soko inayotolewa na TFRA;
- (iii) Ruzuku ya mbolea itatolewa kwa mazao ya chakula na mazao mengine ya kimkakati isipokuwa mazao ya miwa na mkonge;
- (iv) Ruzuku ya Mbolea ya Tumbaku **NPK 10:18:24** itatolewa;
 - a. Kwa kuzingatia ongezeko la bei za mbolea za tumbaku katika soko la dunia, kwa msimu wa 2026, ruzuku ya mbolea itatolewa kwa mbolea ya Tumbaku aina ya NPK 10:18:24, kwa kuzingatia bei halisi ya ununuzi, kwa masharti kwamba kiwango cha ruzuku kitakachotolewa hakitazidi Dola za Marekani 5 kwa mfuko wa kilo 50; na
 - b. Mpango wa ruzuku ya mbolea ya tumbaku utaendeshwa kwa utaratibu wa Serikali kuchangia sehemu ya gharama za ununuzi wa mbolea, kwa kulipia kiasi kisichozidi Dola za Marekani 5 kwa mfuko kilo 50 wa mbolea unaonunuliwa kutoka kwa mzalishaji, kwa kuzingatia pia masharti yaliyowekwa katika aya (a) hapo juu.
- (v) Mpango wa ruzuku hautahusisha mbolea zinazohitajika kwa matumizi mengine nje ya uzalishaji wa mazao ya kilimo. Aidha, muuzaji wa mbolea atapaswa kuomba kibali maalum kutoka TFRA cha kuuza mbolea nje ya mpango wa ruzuku na mbolea hizo hazitakuwa na kifungashio chenye nembo ya **MBOLEA YA RUZUKU**.

2.10 Utoaji wa Adhabu

Katika kuimarisha uwajibikaji, Mwingizaji/Mzalishaji, Wakala wa pembejeo, Mkulima na wadau wengine watakaokiuka utaratibu ulioainishwa katika mwongozo huu watapewa adhabu kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Mbolea Sura ya 378 na Sheria nyingine za nchi; ikiwa ni pamoja na Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 na Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200.

2.11 Utaratibu wa malipo ya ruzuku ya mbolea iliyosambazwa kwa wakulima


Waingizaji/wazalishaji wa mbolea watawasilisha madai ya huduma walizozitoa kwa wakulima kwa utaratibu ufuatao:-

- (i) Kampuni kupitia mfumo wa kidijitali wa ruzuku ya mbolea itaandaa hati ya madai kwa mbolea iliyouzwa kwa wakulima na kuwasilisha TFRA. Hati hiyo iambatishwe na *Delivery Note*, risiti ya kielekitroniki (EFD receipt), orodha ya wakulima walionunua mbolea, aina ya mbolea, vituo vya mauzo na barua ya maombi ya malipo;
- (ii) TFRA itapokea hati ya madai, itahakiki na kufanya usuluhishi wa huduma iliyotolewa na kuidhinisha malipo ya fedha ya ruzuku kwa kampuni husika; na
- (iii) Malipo yatafanyika kwa kuzingatia bei elekezi iliyopangwa katika vituo vya mauzo.

3.0 MUUNDO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU

Katika mwaka wa 2026/2027 utekelezaji wa mpango wa ruzuku utaendelea kutumia Mfumo wa Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo (**Agricultural Inputs Subsidy System**). Mfumo huo unatumika kutambua washiriki (waingizaji/wazalishaji, mawakala na wakulima), kuratibu usambazaji (stock movement) na kuwezesha uwasilishaji wa madai na ulipaji wa ruzuku. Muundo wa utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku umeainishwa kwenye **Kielelezo Na. 1**.

Kielelezo Na. 1: Muundo wa wa utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku



3.1 Utaratibu wa utoaji wa Ruzuku kupitia mfumo wa Kidijitali (*Agricultural Inputs Subsidy System*)

Kutokana na uzoefu wa utekelezaji wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kwa misimu iliyopita, mfumo umeboreshwa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa ruzuku kwa wakulima. Kwa kuzingatia maboresho yaliyofanyika, utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima msimu wa 2026/2027 unazingatia utaratibu ufuatao:-

- (i) Waingizaji/Wazalishaji waliosajiliwa kwa mujibu wa mwongozo na utaratibu wa usajili watapelewa namba za utambulisho kuthibitisha ushiriki wao, sambamba na

namba hizo watapewa uwezo wa kuingia kwenye mfumo kupitia kurasa zao (**portal**);

- (ii) Waingizaji/Wazalishaji wa mbolea watasambaza mbolea kwenye vituo vya mauzo na mawakala waliosajiliwa. Zoezi hilo litahusisha utoaji na upokeaji wa shehena ya kiasi cha mbolea kwenye mfumo (stock in and out). Mzigo (Stock) utafuatiliwa kuanzia ngazi ya uingizaji/uzalishaji mpaka kwa mkulima.
- (iii) Waingizaji/Wazalishaji, Mawakala na vituo vyote vya mauzo havitaruhusiwa kuuza mbolea nje ya utaratibu huu isipokuwa kwa kibali maalum kutoka TFRA;
- (iv) Mkulima aliyesajiliwa na kuhakikiwa taarifa zake ataenda kwa Wakala/Kituo cha usambazaji wa mbolea na kuonesha namba ya utambulisho ili aweze kununua mbolea;
- (v) Mfanyabiashara/Wakala ataingiza namba ya utambulisho wa mkulima kwenye mfumo na kuhakiki taarifa (Jina kamili, eneo analotoka, ukubwa wa shamba, idadi ya mifuko ya mbolea anayopaswa kulipia kwa wakati huo) kabla ya kumuuzia mbolea;
- (vi) Baada ya kuhakiki taarifa za mkulima kwenye mfumo, mfanyabiashara/wakala ataskani *QR code* kwa mbolea inayouzwa na taarifa za mbolea hiyo (aina, kampuni na namba ya mfuko) zitaingia kwenye mfumo wa kidijitali;
- (vii) Mkulima atapokea ujumbe mfupi wenye namba ya siri ya muda (*One Time Password- OTP*) ambayo itatumika ndani ya dakika tano. Mkulima atampa mfanyabiashara/wakala namba hiyo ya *OTP* ili kuthibitisha manunuzi ya mbolea kufanyika;
- (viii) Baada ya kuthibitisha, mfumo utamruhusu wakala kumalizia taratibu za kumuuzia mkulima mbolea;
- (ix) Mkulima atamlipa mfanyabiashara/wakala fedha taslimu kwa ajili ya kiasi cha mbolea anachohitaji kununua kwa kuzingatia bei elekezi iliyotangazwa na Serikali;
- (x) Wakala atatoa risiti ya EFD kwa mkulima baada ya kupokea malipo;
- (xi) Taarifa za mauzo zitaonekana kwenye ukurasa (**portal**) wa Waingizaji/Wazalishaji husika na TFRA;
- (xii) Waingizaji/Wazalishaji watawasilisha hati ya madai TFRA kwa kiasi cha mbolea

ambacho kimeuzwa kwa wakulima;

- (xiii) TFRA itahakiki madai yaliyowasilishwa na kuidhinisha malipo ya fedha ya ruzuku kwa Waingizaji/Wazalishaji ndani ya mwaka fedha husika; na
- (xiv) Malipo kwa Waingizaji/Wazalishaji yatafanyika kwa kuzingatia taratibu za malipo ya Serikali.

3.2 Muundo wa Usimamizi na Uendeshaji

3.2.1. Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea

Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea (*National Fertilizer Subsidy Steering Committee*) itakuwa na wajumbe wafuatao: -

Waziri wa Kilimo	Mwenyekiti
Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo	Katibu
Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha	Mjumbe
Katibu Mkuu wa OWM - TAMISEMI	Mjumbe
Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA	Mjumbe
Afisa Mtendaji Mkuu - NAESA	Mjumbe
Mkurugenzi wa Sera na Mipango - Wizara ya Kilimo	Mjumbe
Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Mazao – Wizara ya Kilimo	Mjumbe
Mkurugenzi Tawala za Mikoa OWM-TAMISEMI	Mjumbe
Mwenyekiti wa Kamati Tendaji	Mjumbe

Katibu wa Kamati anaweza kualika mdau yoyote kushiriki kikao cha Kamati hii kulingana na agenda za kikao husika. Majukumu ya Kamati ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ruzuku yatakuwa:-

- (i) Kuidhinisha vigezo vitakavyotumika kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima;
- (ii) Kuhakikisha kuwa mpango wa ruzuku ya mbolea unapata fedha na zinatolewa kwa wakati;
- (iii) Kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji mpango wa ruzuku ya mbolea; na
- (iv) Kutoa maelekezo mahsusi kwa ajili ya kufanikisha lengo la Serikali la utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima.

3.2.2. Kamati ya Taifa ya Ufuatiliaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea

Kamati ya Taifa ya Ufuatiliaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea itaundwa na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo. Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wasiozidi kumi (10) ambao watakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (i) Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea katika Mikoa na Halmashauri za Wilaya;
- (ii) Kuhakiki kanzidata ya wakulima waliosajiliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (iii) Kufuatilia mwenendo wa uuzaji na matumizi ya mbolea kwa wakulima;
- (iv) Kutathmini taarifa za utekelezaji zinazotolewa na TFRA, Mikoa na Halmashauri za Wilaya na kuiwasilisha kwa Kamati ya Taifa ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea (National Fertilizer Subsidy Steering Committee); na
- (v) Kubaini changamoto zilizopo na kuzipatia ufumbuzi kwa kushauriana na Wizara ya Kilimo, TFRA, Sekeretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku.

3.2.3. Kamati Tendaji (Technical Committee)

Kamati Tendaji itasimamia utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea na itaundwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA. Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa TFRA, Katibu na Wajumbe wasiozidi kumi (10) na itakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (i) Kusajili Kampuni na wafanyabishara wa mbolea watakaoshiriki katika mpango wa ruzuku;
- (ii) Kutoa elimu ya mfumo wa ruzuku kwa wadau;
- (iii) Kuratibu uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea;
- (iv) Kuwa Sekretarieti ya Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea;
- (v) Kuratibu shughuli za uhamasishaji wa mpango wa ruzuku (*program promotion*);
- (vi) Kuratibu shughuli za ufuatiliaji na tathmini; na
- (vii) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa mwezi, robo mwaka,

nusu mwaka, na mwaka na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Taifa ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea (National Fertilizer Subsidy Steering Committee).

4.0 NGAZI ZA UTEKELEZAJI NA WAJIBU WA WADAU

Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea unahusisha ngazi mbalimbali za utekelezaji na majukumu yake. Ngazi zitakazohusika katika mpango wa ruzuku ni Wizara ya Kilimo, TFRA, Bodi za Mazao, Wakala ya Taifa ya Huduma za Ugani wa Kilimo (NAESA), Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Waingizaji/Wazalishaji wa Mbolea, Mawakala wa Mbolea, Taasisi za Fedha na Wakulima. Majukumu ya ngazi za utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

4.1 Wizara ya Kilimo

Majukumu ya Wizara ya Kilimo yatakuwa ni:-

- (i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Ruzuku ya Mbolea;
- (ii) Kufuatilia upatikanaji wa fedha za ruzuku;
- (iii) Kuunda Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea (National Fertilizer Subsidy Steering Committee) na Kamati ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathimini ya Mpango wa Ruzuku ya Mbolea;
- (iv) Kutoa Mwongozo wa Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku;
- (v) Kutoa maelekezo yatakayowezesha utekelezaji wa mpango wa ruzuku;
- (vi) Kushughulikia masuala mengine yatakayohitaji maamuzi ya Wizara; na
- (vii) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji ili kuhakikisha kuwa mpango wa ruzuku unatekelezwa kwa mujibu wa Mwongozo huu.

4.2 Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)

Majukumu ya TFRA yatakuwa ni:-

- (i) Kusajili wakulima watakaonufaika na ruzuku ya mbolea kwa kushirikiana na Bodi za Mazao, NAESA, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (ii) Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea;

- (iii) Kuunda Kamati Tendaji kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kwa kadri itakavyohitajika;
- (iv) Kuandaa makisio ya mahitaji ya mbolea kwa mikoa yote ya Tanzania Bara;
- (v) Kuingia mikataba ya makubaliano na Waingizaji/Wazalishaji wa mbolea waliosajiliwa kwa ajili ya kuuza mbolea kwa wakulima katika mpango wa ruzuku;
- (vi) Kuingia mikataba na watoa huduma mbalimbali katika utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea;
- (vii) Kupanga na kutangaza bei elekezi ya mbolea na kusimamia utekelezaji wake;
- (viii) Kushirikiana na wadau wa mbolea katika kufanikisha utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea; kutoa elimu kwa umma kuhusu utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine muhimu; kufungua na kusimamia akaunti maalum zitakazotumika kupokea na kulipa fedha za ruzuku kwa watoa huduma;
- (ix) Kuidhinisha malipo ya ruzuku ya mbolea iliyouzwa kwa wakulima;
- (x) Kushirikiana na Taasisi za Fedha kufanya usuluhishi wa malipo ya ruzuku ya mbolea mara kwa mara;
- (xi) Kutoa adhabu na faini ikiwemo kumsimamisha kwenye mfumo mfanyabiashara/mkulima atakayebainika kufanya udanganyifu kinyume na taratibu zilizoainishwa kwenye Mwongozo huu au kwenda kinyume na Sheria za nchi ikiwemo Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009 na Kanuni zake;
- (xii) Kupokea na kushughulikia malalamiko/changamoto za utekelezaji zinazohusu mpango wa ruzuku ya mbolea na kuwasilisha taarifa Wizara ya Kilimo;
- (xiii) Kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima; na
- (xiv) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kila mwezi na kuiwasilisha Wizara ya Kilimo.

4.3 Bodi za Mazao na Wakala ya Taifa ya Huduma za Ugani wa Kilimo (NAESA)

Majukumu ya Bodi za Mazao na Wakala ya Huduma za Ugani wa Kilimo (NAESA) yatakuwa kama ifuatavyo:-

- (i) Kusajili/kuhakiki wakulima katika mfumo wa Kidijitali kwa kushirikiana na TFRA, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (ii) Kuainisha mahitaji ya mbolea kwa mazao husika; na
- (iii) Kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya mbolea kwa wakulima.

4.4 Sekretarieti za Mikoa

Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kusimamia Halmashauri zote zilizopo kwenye mikoa husika ili zitekeleze kwa ufanisi majukumu yake kwa mujibu wa mwongozo wa mpango wa ruzuku;
- (ii) Kushirikiana na TFRA katika kuhamasisha na kusajili wakulima ikiwa ni pamoja na kuhakiki kanzidata ya wakulima waliosajiliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (iii) Kufanya tathimini ya mahitaji ya mbolea na kuyawasilisha TFRA;
- (iv) Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea; na
- (v) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kila mwezi na kuiwasilisha Wizara ya Kilimo na TFRA.

4.5 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo: -

- (i) Kushirikiana na wadau wengine kusajili/kuhakiki taarifa za wakulima na kuandaa kanzidata ya wakulima katika ngazi ya kijiji/mtaa;
- (ii) Kusimamia utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa kuzingatia bei elekezi zitakazotangazwa na Serikali;
- (iii) Kupokea maoni kutoka kwa wafanyabiashara wa mbolea kuhusu hali ya usambazaji wa mbolea na kutoa mapendekezo kwa TFRA pale inapotokea changamoto za usambazaji;
- (iv) Kutoa elimu kwa wadau wote kwenye ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu mpango wa ruzuku ya mbolea;
- (v) Kusimamia matumizi sahihi ya mbolea ya ruzuku kwa wakulima ili kuhakikisha

kuwa mbolea inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa; na

- (vi) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kila mwezi na kuiwasilisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

4.6 Waingizaji/ Wazalishaji wa Mbolea

Kampuni zinazojihusisha na uingizaji na uzalishaji wa mbolea zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (i) Kujisajili kushiriki katika mpango wa ruzuku;
- (ii) Kuingiza nchini au kuzalisha mbolea zitakazouzwa kwa bei ya ruzuku kwa wakulima;
- (iii) Kusaini/Kuhuisha mikataba ya utoaji wa huduma katika mpango wa ruzuku;
- (iv) Kuwasilisha TFRA orodha ya mawakala watakaofanya nao kazi ya usambazaji wa mbolea;
- (v) Kuingia mikataba na wafanyabiashara/mawakala wa kusambaza mbolea ya ruzuku kwa wakulima;
- (vi) Kuingiza kwenye mfumo wa kidijitali taarifa za mbolea iliyozalishwa/kuingizwa nchini na kusambazwa kwenye vituo vya mauzo au kuuzwa kwa wakala kwenye mpango wa ruzuku;
- (vii) Kuhakikisha mbolea ya ruzuku inafungashwa katika mifuko ambayo imeandikwa "MBOLEA YA RUZUKU"
- (viii) Kuwasimamia mawakala waliowateua ili kuhakikisha wanafikisha na kuuza mbolea kwa wakulima kwa utaratibu uliowekwa;
- (ix) Kuwasilisha hati za madai ya fedha za ruzuku kwa TFRA baada ya mbolea kuuzwa kwa wakulima;na
- (x) Kuhakikisha mawakala wanakuwa na mbolea wakati wote wa msimu.

4.7 Mawakala (Agrodealers) wa Mbolea

Majukumu ya Mawakala (Agrodealers) wa mbolea yatakuwa ni:-

- (i) Kuingia mkataba na Waingizaji/Wazalishaji wa mbolea kwa ajili ya kushiriki

katika mpango wa ruzuku

- (ii) Kuhakikisha wanaanzisha vituo vya mauzo karibu na wakulima ili kupunguza umbali wa kufuata mbolea;
- (iii) Kutumia mfumo wa kidijitali kuuza mbolea kwa mkulima aliyesajiliwa;
- (iv) Kutoa taarifa kwa Mamlaka kuhusu viashiria vya udanganyifu vinavyojitokeza wakati wa kuuza mbolea; na
- (v) Kuhakikisha mbolea ya ruzuku inasambazwa/kuuzwa kwa wakulima kwa bei ya ruzuku wakati wote wa msimu wa 2026/2027.

4.8 Taasisi za Fedha

Majukumu ya Taasisi za Fedha yatakuwa ni:-

- i) Kushirikiana na TFRA na Serikali za Mitaa kufanya usajili wa wakulima;
- ii) Kupokea fedha za ruzuku ya mbolea kutoka Serikalini kupitia akaunti maalum kwa ajili ya kuwezesha malipo yanayostahili;
- iii) Kufanya malipo kwa Kampuni za mbolea zilizotoa huduma kwa wakulima baada ya kupata idhini ya TFRA; na
- iv) Kushirikiana na TFRA kufanya usuluhishi wa malipo ya ruzuku ya mbolea mara kwa mara.

4.9 Wakulima

Majukumu ya wakulima watakaonufaika na ruzuku ya mbolea yatakuwa ni:-

- (i) Kuhakikisha kuwa amesajiliwa/kuhakiki taarifa zake kwenye mfumo kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kupewa namba maalum ya utambulisho;
- (ii) Kutunza namba ya utambulisho ya ruzuku ya mbolea;
- (iii) Kuonesha namba ya utambulisho aliyopewa wakati wa usajili anapokwenda kununua mbolea kwa wakala;
- (iv) Kuthibitisha manunuzi kwa kutoa namba ya siri (One Time Password-OTP) kwa wakala anaponunua mbolea;
- (v) Kununua mbolea kwa bei elekezi iliyotangazwa na Serikali;

- (vi) Kuhakikisha mbolea anayonunua kwa bei ya ruzuku anaitumia kwenye shamba lake; na
- (vii) Kutoa taarifa kwa Mamlaka pale anapohisi kuna viashiria vya udanganyifu.

5.0 MAMBO YA KUZINGATIA

Katika utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kwa wakulima, Wadau wanasisitizwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

- (i) Kila mkulima anapaswa kujisajili kwenye mfumo ili kupata namba ya kununulia mbolea;
- (ii) Kila mkulima anapaswa kutunza namba yake ya kununulia mbolea na haitaruhusiwa kutumiwa na mkulima mwingine;
- (iii) Mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa 2026/2027 utafikia ukomo tarehe 30 Juni, 2027;
- (iv) Mbolea ya ruzuku itumike kwa ajili ya matumizi ya kilimo pekee na si vinginevyo, kwa mahitaji ya matumizi ya mbolea nje ya kilimo wadau watapaswa kuomba kibali maalum kutoka TFRA;
- (v) Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kubaini changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi;
- (vi) Ushauri, maoni na malalamiko kuhusu utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya mbolea uwasilishwe katika Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Wizara ya Kilimo kupitia namba 0733 800 200 na 0800 110 153/4 kuanzia saa 1:30 Asubuhi hadi saa 4:00 Usiku; na
- (vii) Kwa upande wa vikundi vya wakulima vilivyosajiliwa, ruzuku itatolewa kwa kikundi kinacho miliki shamba kwa pamoja na si kwa mwanakikundi mmoja mmoja.

6.0 MAREKEBISHO

Mwongozo huu unaweza kuboreshwa wakati wowote kwa kadri ya mahitaji.

7.0 HITIMISHO

Mwongozo huu ukitumiwa vizuri katika ngazi zote za utekelezaji utawezesha azma ya Serikali ya kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima katika msimu wa kilimo wa 2026/2027. Kila mdau aliyetajwa katika Mwongozo huu anatakiwa kuwajibika ipasavyo ili kuwezesha malengo ya Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kufikiwa. Vilevile, Mwongozo huu utatumika sambamba na Mwongozo wa Mpango Maalumu wa Ruzuku ya Mbolea kwa Wazalishaji wa Ndani wa mwaka 2026/2027.